**SEHEMU YA C: HADITHI FUPI**
**TUMBO LISILOSHIBA NA NYINGINE.**
**(ALIFA CHOKOCHO NA DUMU KAYANDA)**

**JIBU SWALI LA 4 AU5**

4. " Wenye jadi kubeli na wachochole wanapitia chini ingawa wamo chuo kimoja na wanafanya masomo mamoja."
   (a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama4)

   (b) Eleza sifa **nne** za anayehusishwa na kauli hii. (alama4)

   (c) Jadili masaibu yanayomkumba mzungumzaji katika maisha yake. (alama4)

for more free revision content visit www.freekcsepastpapers.com

(d) Thibitisha jinsi wenye jadi kubeli wanavyopitia juu nao wachochole wakipitia chini kwa mujibu wa hadithi husika. (alama8)

5. (a) "Mame Bakari"
Kwa mujibu wa hadithi hii, ubahaimu anaotendewa mwanamke unakuwa na athari mbaya kwake. Onyesha kwa mifano mwafaka. (alama10)

for more free revision content visit www.freekcsepastpapers.com

(b) " Masharti ya Kisasa"
"......Mapenzi ni mateso, ni utumwa, ni ukadamizaji, ni ushabiki usio na maana"
Thibitisha ukweli wa kauli hii kama inavyojitokeza kwenye hadithi. (alama10)

for more free revision content visit www.freekcsepastpapers.com

## SEHEMU YA D: USHAIRI

**6. <u>SOMA SHAIRI LIFUATALO KISHA UJIBU MASWALI.</u>**

Hukuja hapa kwa wingi,
Vitimbi vya kila namna,
Kunambia nikuruzuku,
Kimwana awe mwenzio,
Hukumtwaa mwanangu,
Kisema mno walavu,
Vipi wangeuza ngoma,
Mapepo wampigia?

Siwe uloandaa,
Harusi ya kukata na shoka,
Masafu ya magari, yakilalama jua kali,
Hadi kanisani kungia, mimbari wa kusimama,
Kasema utamuezi, hadi yenu mauko?
Vipi jicho lageukia, mitaani vipaa mwitu?

Hukunambia we fidhuli,
Mwanangu utamtunza?
Taandamana naye daima,
Ja chanda na pete?
Hukumwonjesha tamu, ya ulaghai huyuno,
Vipi wamtezea shere, mwanangu?

Lini taacha dhuluma hizino humfanyiazo,
Tuchukua lini majukumu,
Ya kumlea na vifaranga?
Huachi kulia u waya,.
Wanao kitelekeza
Nadhiri zako za nitakipu promise,
Zi wapi mwana balaa?

Lini tafumbua maozi, uone huyu nduli,
Alotwala wengi wapendi,
Kwa jicho la nje kuwangia,
Imeanguka miamba mingapi, nayo ngangania kufia dodani,
Zinduka mwana zinduka,
Ailayo waangamiza.

**<u>Maswali</u>**

(a) Hili ni shairi huru. Thibitisha. (alama2)

for more free revision content visit www.freekcsepastpapers.com

(b) Mwandishi anaibusha masuala kadhaa ya kijamii. Yadokeze. (alama2)

(c) Bainisha nafsineni katika shairi hili. (alama1)

(d) Eleza toni ya utungo huu. (alama1)

(e) Bainisha matumizi ya:- (alama2)

(i) Mistari mishata

(ii) Mistari kifu / toshelezi

(f) Eleza kwa kutoa mifano mbinu za kifasihi zilizotumika katika ushairi huu. (alama3)

(g) Eleza vile mshairi alivyotumia idhini ya kishairi katika utungo huu. (alama3)

(h) Bainisha umuhimu wa masuala ya balagha yaliyoyumika katika ushairi huu. (alama2)

for more free revision content visit www.freekcsepastpapers.com

(i) Andika ubeti wa tatu kwa lugha tutumbi. (alama4)

**7. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata:**

Mungu naomba subira, subira nayo imani
Imani iliyobora, bora hapa duniani.

Duniani mwa kombora, kombora nayo hiani
Hiani pamwe ukora wenye kuhini.

Kuhini kwenye kiburi, kiburi na ufidhulu
Ufidhulu wa kudhuri, kudhuri wangu muwili
Muwili hata kidari, kidari kuwa thakili
Thakili kisinawiri, kisinawiri misuli.

Misuli kuwa hafifu, hafifu kama muwele
Muwele wa hilafu, hitilafu ya nduwele
Nduwele kutakilifu, kutakilifu milele
Milele kutoniafu, kutoniafu na vishale.

Vishale vinatomele, vitomele vikwato
Vikwato pia maole, maole kufanya mito
Mito ya matozi tele, tele mithili kitoto
Kitoto kilo vipele, vipele vyenye fiakuto.

Fukuto lanipa neno, neno hili kutamka
Kutamka wazi vino, vino subira kutaka
Kutaka imani mno, n'sipate wahaka
Wahaka wa matukano, matukano na mashaka.

Mashaka haya ya leo, leo yawe yamepita
Yamepita na vilio, vilia vipishe nyota

for more free revision content visit www.freekcsepastpapers.com

Nyota njema ing'arao, ing'arao kunitika

Kunitika salamani, salamani nikadata

**Maswali**

(a) Kwa nini nafsi neni anaomba subira na amani (alama1)

(b) Shairi hili ni la aina gani kwa kuzingatia; (alama3)

(i) Mpangilio wa maneno

(ii) Mpangilio wa vina

(iii) Idadi ya mishororo

(c) Kwa kutolea mifano eleza mbinu mbili za lugha zilizotumika katika shairi. (alama4)

(d) Andika ubeti wa tatu kwa lugha nathari. (alama4)

(e) Eleza umuhimu wa urudiaji wa maneno katika shairi hili (alama2)

for more free revision content visit www.freekcsepastpapers.com

i) Kwa kutolea mifano, eleza jinsi uhuru wa kishairi ulivyotumiwa kutekeleza arudhi. (alan

## SEHEMU YA E:

## 8. FASIHI SIMULIZI

We malaika wangu
Uloshuka toka mbinguni
Mbingu kapasua kwa heri
Siku nipokukopoa
Ulinitia furaha iliyopasua kifua
Tabasamu kipajini pako
Ilinitia tumaini, ikanisahaulisha zingizi
Ikayayeyusha madhila, ya utasa wa miaka kumi
Ikapeperusha mbali, cheko la ukewenza.

Sasa napolia, wanitonesha jeraha
Wanirejesha misri, kwa vitimbi vya Firauni
Kwa vitisho kuahidiwa, hadi mbingu
Lipofunguliwa milango ya heri.

Silie mwana silie, walimwengu watakusuta,
Tangu hapo tanabahi
Vidume humu mwenu
Kulia hazikuumbiwa,
Machozi na kekevu ni za kike fahamu,
ogoo halii daima huwika
ikikuona kigugumika hivi wanitia hangaiko
maini kuzima
haifu kiandama
yo kutia hamaniko,
nipigania nani?
esi king'ang'ania
gu kujitwalia?

for more free revision content visit www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**

(a) Thibitisha aina ya utungo huu. (alama2)

(b) (i) Bainisha jinsia inayoongelewa kwenye utungo huu. (alama1)

(iii) Thibitisha jibu lako la hapo juu (i) (alama1)

(c) (i) Eleza nafsineni kattika utungo huu. (alama1)

(ii) Toa sababu mbili kuthibitisha jibu lako hapo juu (i) (alama1)

(d) Eleza sifa **tano** za utungo huu. (alama5)

for more free revision content visit www.freekcsepastpapers.com

(e) Huku ukitoa mifano, bainisha vipengele sita vya kimtindo ambapo nafsineni imetumia kufanikisha uwasilishaji wa utungo huu. (alama6)

(f) Eleza majukumu tano ya utungo huu. (alama5)

for more free revision content visit www.freekcsepastpapers.com